

**SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, 1982**

**SURA YA 290**

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(k) na 16(1)*

**SHERIA NDOGO ZA USHURU WA SOKO NA MAGULIO ZA HALMASHAURI YA  
WILAYA YA MUHEZA, 2012**

**SEHEMU YA I  
MASHARTI YA MWANZO**

- |  |    |  |
|--|----|--|
| Jina na tarehe<br>ya kuanza<br>kutumika            | 1. | Sheria Ndogo hizi ziiitwe Sheria Ndogo za Ushuru wa Soko za Halmashauri ya Wilaya ya Muheza za Mwaka 2012 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.   |
| Matumizi   | 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmshauri ya Wilaya ya Mkinga.  |
| tafsiri<br>Sura ya 290<br>ya Sheria za<br>Tanzania | 3. | <p>Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-<br/>“Sheria” maana yake ni sheria za Fedha za Serikali za Mitaa za Mwaka 1982;</p> <p>“Mwenyekiti”</p> <p>(a) Linapotumika kuhusiana na Halmashauri ya Wilaya maana yake ni mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya;</p> <p>(b) Linapotumika kuhusiana na Kijiji, maana yake ni Mwenyekiti wa kijiji;</p> <p>(c) Linapotumika kuhusiana na Kitongoji, maana yake ni Mwenyekiti wa kitongoji;</p> <p>“Afisa muidhiniwa” maana yake ni mtu ambaye amejiriwa na au ambaye yumo katika utumishi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na ambaye ameidhiniwa na Halmashauri kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria ndogo hizi;</p> <p>“Ushuru” maana yake ni ushuru wa soko;</p> <p>“Masoko yaliyoanzishwa” maana yake ni orodha ya masoko yaliyoorodheshwa katika jedwali la pili la sheria Nsogo hizi;</p> <p>“Soko” maana yake ni sehemu yoyote ya soko inayotumiwa na watu kwa kuuza na kununua mazao au bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na maduka ndani na nje ya soko, vioski, na meza kuzunguka eneo linalotambuliwa na Halmashauri kama soko na litajumuisha eneo lolote la wazi la sokoni hapo na itajumuisha magulio na minada;</p> |

“vizimba” maana yake itajumuisha jengo lolote, chumba, kioski, duka ndani ya soko au kuzunguka eneo la soko ambalo linatumika kwa madhumuni ya kuuzia mazao au bidhaa chini ya sheria ndogo hizi ikiwa kizimba hicho kimejengwa na Halmashauri au mfanyabiashara;

“Mmiliki wa kizimba” maana yake ni mtu yeyote aliyeingia mkataba na Halmashauri wa kutumia kizimba sokoni na itajumuisha mtu yeyote aliyeajiriwa na mmiliki wa kizimba katika katika kizimba husika kwa kuuzia mazao au bidhaa chini ya Sheria ndogo hizi;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya au mtu yeyote aliyeteuliwa kufanya kazi za Mkurugenzi.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa:

## **SEHEMU YA II JINSI YA KUTOZA USHURU**

Ushuru  
Sheria na. 15 ya  
Mwaka 2003

- 4
- (1) Halmashauri itatoza ushuru utakaojulikana kama ushuru wa soko utakaolipwa na mmiliki yeyote wa kizimba kilichopo sokoni kama ilivyobainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi;
  - (2) Bila ya kuathiri maelezo ya jumla ya sheria ndogo 4(1) hapo juu kila, mmiliki wa kizimba ataingia mkataba na Halmashauri ili kuhlalisha umiliki wa kizimba hicho kisheria.;
  - (3) Mfanyabiashara yeyote anayetumia eneo la soko, Gulio au Minada iliyopo katika soko lolote lililopo katika eneo la mamlaka ya Halmashauri atawajibika kulipa ushuru wa soko kwa kiwango kilichobainishwa katika jedwali la kwanza la sheria ndogo hizi;
  - (4) Ushuru utatozwa kwa mfanyabiashara yeyote anayefanya biashara katika eneo la Soko bila kujali kwamba eneo husika limejengwa na Halmashauri au la,  
Maadamu tu Halmashauri iwe imelitangaza eneo husika kuwa ni eneo la soko.
  - (5) Si ruhusa kwa mtu yeyote kufanya biashara katika eneo ambalo halijatengwa na Halmashauri kwa minaajili ya kufanya shughuli za soko tofauti na orodha ya masoko iliyoainishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi. Na kwamba si ruhusa kwa mtu yoyote kufanya biashara kiholela.

wakala

- 5.
- (1) Halmashauri inaweza kutangaza zabuni ya ukusanyaji ushuru wa Soko na kumteua wakala ikiwa ni mtu binafsi, kampuni au taasisi ambaye ataingia mkataba wa uwakala na Halmashauri wa ukusanyaji wa ushuru huo.
  - (2) Kwa madhumuni ya kurahisisha ukusanyaji na kuepuka gharama za ukusanyaji wa ushuru huu, pale ambapo Halmashauri itaona inafaa kufanya ubinafsishaji wa ukusanyaji wa ushuru wa soko, itawajibika kufanya uchambuzi wa kina utakaobainisha wazi kiasi cha ushuru unaoweza kupatikana kuhusiana na chanzo hicho na kamwe Halmashauri

haitaruhusiwa kuingia mkataba na wakala kabla haijafanya uchambuzi wa kina kuhusiana na uwezo wa upatikanaji fedha wa chanzo hicho.

- (3) Wakala atakayeteuliwa na Halmashauri kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria ndogo hizi, atawajibika kusimamia ukusanyaji huo kwa viwango vilivyoainishwa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi na kamwe hataruhusiwa kutoza viwango tofauti na vilivyobainishwa chini ya Sheria Ndogo hii.
- (4) Mtu yeyote atakayeteuliwa kama wakala chini ya Sheria ndogo hii, atakuwa na majukumu ya kukusanya ushuru na kumshitaki mtu yeyote atakayeshindwa kwa makusudi kulipa ushuru anaotakiwa kulipa kwa wakala huyo kwa muda unaotakiwa katika Mahakama yenye Mamlaka ya kusikiliza shauri hilo kama madai.
- (5) Wakala atakuwa na majukumu kwa Halmashauri yafuatayo:-
  - (a) Kukusanya na kupokea ushuru kwa kiwango kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri katika eneo ambalo ameteuliwa kukusanya ushuru husika;
  - (b) Kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;
  - (c) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria ndogo hizi;
- (6) Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi, kwa Wakala yeyote aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi:-
  - (a) Akishindwa bila sababu ya msingi kuwasilisha kiwango cha fedha kwa kiwango kilichoainishwa katika mkataba wa uwakala;
  - (b) Akiwa anafahamu kiwango kinachostahili kutozwa kutoka kwa wafanyabiashara sokoni na kwa makusudi akakusanya zaidi ya kiwango husika; na
  - (c) Kwa makusudi akishindwa kutekeleza lolote analowajibika kulitekeleza kitendo ambacho kitaathiri mapato hayo.

Usimamizi wa soko

6. (1) Soko litakuwa chini ya usimamizi wa Afisa wa Soko ambaye amechaguliwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kutekeleza shughuli zote za usimamizi wa soko ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa taratibu, masharti na kanuni za soko zinafuatwa;
- (2) Mtu yeyote ambaye anatumia soko anapaswa kufuata maelekezao halali atakayopewa na Afisa wa Soko ambaye yupo kwa niaba ya Halmashauri kwa usimamizi wa usafi, taratibu na Sheria ndogo za Ushuru wa Soko ili kufanikisha biashara zinazoendeshwa au zinazofanyika sokoni.
- (3) Endapo mtu yeyote atashindwa, atadharau au atakataa bila ya sababu ya msingi maelekezo halali atakayopewa na Afisa wa Soko, Afisa huyo anaweza kumuondoa mtu huyo sokoni;

- (4) Maelekezo yatakayotolewa na Afisa wa Soko yatajumuisha-
- (a) kuzuia mazao au bidhaa ambazo kwa maoni ya Afisa huyo zinaweza kuleta madhara au kuleta wadudu zisiletwe sokoni;
  - (b) kuhakikisha kwamba taratibu za usafi kwa wamiliki mbalimbali wa vizimba zinafuatwa.
- Muda wa soko kuwa wazi 7. Soko litakuwa wazi kuanzia saa 12 asubuhi mpaka saa moja usiku kila siku.
- Wajibu wa watumiaji soko 8. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza au kununua mazao au bidhaa nyingine yoyote sokoni kwa zaidi ya muda ulioelekezwa katika Sheria ndogo ya 8 hapo juu.
- Mgawanyo wa vizimba sokoni 9. (1) Soko litagawanyika katika Vizimba, vyumba, stoo au stendi kutegemeana na uamuzi wa halmashauri wa mara kwa mara.
- (2) Maombi ya kutumia vizimba, stoo au vyumba sokoni yatatumwa kwa Afisa wa soko na maombi hayo yatakuwa kwa utaratibu wa siku au mwezi.
- (3) Maombi yoyote ya matumizi ya vizimba yatazingatiwa maelezo ya Sheria ndogo hizi na masharti yatakayowekwa na Halmashauri mara kwa mara.
- (4) Vipaumbele kwa mgao wa vizimba utakuwa kutokana na mpangilio wa maombi yalivyopokelewa.
- (5) Ushuru utakaolipwa kwa kizimba utatangazwa katika sehemu ya wazi sokoni na hautapungua gharama zilizoordheshwa katika jedwali la kwanza la Sheria ndogo hizi.
- Maadam tu badala ya ushuru wa kawaida ulionyeshwa katika jedwali la pili la sheria Ndogo hizi kwa siku au mwezi lakini usipungue ushuru uliobainishwa katika Sheria ndogo hizi.
- Matumizi ya kizimba 10. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza mazao au bidhaa zozote sokoni kama ilivyoelezwa chini ya Sheria Ndogo ya 9 hapo juu isipokuwa katika kizimba ambacho ameomba na kupangiwa na Afisa wa Soko.
- Mnada sokoni 11. Halmashauri inaweza kuamua kuwa aina fulani ya mazao au bidhaa ziuzwe kwa mnada na maelekezo yatakayotolewa na Afisa wa Soko.
- Viwango vya ubora wa bidhaa zinazouzwa sokoni na uwezo wa Afisa mteule kufafanua viwango 12. (1) Halmashauri itafafanua viwango vya ubora wa mazao au bidhaa ambavyo vinafaa kuuzwa sokoni, viwango ambavyo havijaelezwwa katika Sheria yoyote andikwa na pale ambapo viwango vimefafanuliwa, hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kuuza au kuuziwa mazao au bidhaa yoyote ila yenye ubora wa viwango vilivyofafanuliwa.
- (2) Afisa Soko anaweza kuzuia uuzaji wa bidhaa au mazao yoyote ambayo hayajakidhi viwango vya ubora uliofafanuliwa.
- (3) Ikiwa viwango vya ubora wa mazao au bidhaa zozote hazijafafanuliwa kama ilivyoelezwa chini ya sheria ndogo ya 13(1) hapo juu, Afisa Soko atakuwa na uwezo wa kufafanua viwango hivyo na hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kuuza au kununua mazao au bidhaa ila kwa kiwangokilichowekwa na Afisa Soko.

- (4) Kwa madhumuni ya kuzuia uchafu au madhara mengine yoyote mnunuzi wa mazao yoyote atawajibika kuhifadhi bidhaa alizozinunua katika mifuko.

**SEHEMU YA III**  
**MAKOSA, ADHABU NA JINSI YA KUCHUKUA**  
**HATUA KISHERIA**

- |  |   |
|--|---|
| Deni   | 13. (1) Ushuru, ada au faini yoyote ambayo Halmashauri inadai kwa mtu yoyote, kikundi cha watu, kampuni au Taasisi chini ya Sheria ndogo hizi itakuwa ni deni la Halmashauri na litalipwa kutoka kwa mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au Taasisi kupitia kwa Mkurugenzi au Afisa yeyote aliyeidhiniwa chini ya Sheria ndogo hizi kwa niaba ya Mkurugenzi.                |
|  | (2) Bila ya kuathiri maelezo ya jumla ya Sheria Ndogo ya 13(1) hapo juu, kuhusiana na jinsi ya kudai deni lolote la Halmashauri, ikiwa Afisa yeyote aliyeidhiniwa na Mkurugenzi atafungua shauri katika Mahakama yenye Mamlaka ya kusikiliza shauri na ataandaa hati ya malalamiko ambayo itaeleza uzito wa kosa na maombi.   |
|  | (3) Kutokana na hati ya madai ya deni la Halmashauri pamoja na faida 10% ya deni hilo iliyoandaliwa dhidi ya mdaiwa yeyote kupelekwa Mahakamani.  |
|  | (4) Kila hati ya madai ambayo itapelekwa Mahakamani <sup>9</sup> kwa njia ambayo imeelezwa katika Sheria ndogo hi, itakuwa ni uthibitisho kamili wa madai yaliyoelezwa katika hati hiyo.  |
| Uwezo wa mkurugenzi kumlipisha mkusanya ushuru | 14. Bila ya kuathiri maelezo ya jumla ya Sheria Ndogo ya 13 Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote anayedaiwa na Halmashauri chini ya Sheria ndogo hizi ikiwa mdaiwa huyo amekiri kwa maadishi kuwa atalipa deni analodaiwa pamoja na faini na kasha atapatiwa stakabadhi ya malipo hayo.  |
| Mdaiwa anaposhindwa kulipa deni                | 15. Ikiwa mdaiwa yeyote atatozwa faini chini ya Sheria ndogo ya 14 hapo juu na akashindwa kulipa deni hilo kwa wakati, Mahakama itaendelea kusikiliza shauri hilo kama kawaida inavyosikiliza mashauri mengine na itatumia mamlaka yake eidha iongeze adhabu au itoe adhabu ya kifungo kwa mdaiwa yeyote kwa muda usiopungua miezi sita au vyote kwa pamoja faini na kifungo. |
| Wajibu wa kutoa taarifa                        | 16. (1) Mtu yeyote ambaye anawajibika kutoa taarifa kuhusiana na malipo ya ushuru anawajibika kutoa taarifa hizo kama alivyotarajiwa kwa halmashauri, Kijiji, mkusanya ushuru au Wakala kuhusiana na Ukusanyaji ushuru.   |
|  | (2) Kwa madhumuni ya kupata taarifa chini ya Sheria ndogo ya 16(1) hapo juu, Halmashauri, Kijiji, mkusanya ushuru, Wakala kutegemeana na yeyote anayehusika na utoaji wa wito huo, inaweza kumuita mtu yeyote kufika mbele yake katika muda na mahali ambapo pametajwa katika barua ya wito.  |

- Kukataa kutoa taarifa
17. (1) Mtu yeyote ambaye atatakiwa kutoa taarifa chini ya Sheria Ndogo ya 16 ya Sheria Ndogo hizi, kwa makusudi atatoa taarifa ya uongo au amejaribu kutoa taarifa ya uongokwa Halmashauri, Kijiji, Wakala, Mlipa ushuru juu ya suala lolote linalohusiana na ukusanyaji ushuru, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya elfu hamsini au kifungo cha miezi sita au vyote viwili kwa pamoja faini na adhabu ya kifungo hicho.
- (2) Mtu yeyote ambaye ametakiwa kutoa taarifa chini ya Sheria Ndogo ya 16 ya Sheria Ndogo hizi, amedharau, amekataa au bila ya sababu za msingi ameshindwa kutoa taarifa zinazotakiwa atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya elfu hamsini au kifungo cha miezi mitatu au vyote viwili kwa pamoja faini na adhabu ya kifungo hicho.
- (3) Mtu yeyote ambaye ametakiwa kufika mbele ya Halmashauri, Kijiji, mkusanya ushuru au Wakala atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya elfu hamsini au kifungo cha miezi mitatu au vyote viwili kwa pamoja faini na adhabu ya kifungo hicho.
- Kukusanya ushuru bila ruhusa
18. Mtu yeyote ambaye-
- (a) hajaruhusiwa na Halmashauri au Kijiji kwa maadishi kukusanya ushuru unaokusanywa chini ya sheria ndogo hizi;
- (b) amekusanya au amejaribu kukusanya ushuru kwa kiwango ambacho hakijatajwa chini ya Sheria ndogo hizi;  
 atakuwa ametenda kosa chini ya sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia ya kufanya kosa hilo, atalipa faini ya shilingi elfu hamsini au kifungo cha miezi sita au vyote viwili kwa pamoja faini na adhabu ya kifungo hicho.
- Hatua za kisheria
19. Mashauri yote kuhusiana na malipo ya ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi au kuhusiana na adhabu yoyote chini ya Sheria Ndogo hizi, yanaweza bila kuathiri haki ya mtu yeyote au mamlaka nyingine ya kufungua shauri la jinai, litafunguliwa na Halmashauri kuhusiana na makusanyo ya ushuru mbele ya Mahakama yoyote yenye Mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.
- Hati ya Kukamata Mali
20. (1) Bila ya kuathiri Sheria ndogo ya 11, 12 na 13, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kisheria kuomba katika Mahakama yenye Mamlaka katika eneo la Halmashauri, kwa kutumia hati iliyopo katika jedwali la kwana la Sheria Ndogo hizi, hati ambayo itaonyesha jina la mlipa ushuru na anuani ya mlipa ushuru na kumtaka mlipa ushuru huyo kulipa deni na faida anayodaiwa kulingana na Sheria ndogo hizi.
- (2) Hati atakayopewa mlipa ushuru na mahakama itakuwa na mamlaka ya mamlaka kisheria ya kukamata na kuuza mali inayoondosheka ya Mlipa ushuru na kila hati ya madai ambayo itapelekwa mahakamani kwa nia ambayo imeelezwa katika Sheria Ndogo hizi, itakuwa ni uthibitisho kamili wa maelezo ya madai yaliyoelezwa chini ya hati hiyo.

Makosa na  
adhabu

21. Mtu yeyote ikiwa ni mnunuzi, muuzaji, wakala au mkusanya ushuru ambaye:-
- (a) ameshindwa, amedharau, au amekaidi kulipa ushuru chini ya Sheria ndogo hizi;
  - (b) ameshindwa, amedharau, au amekaidi kuwasilisha ushuru aliokusanya kwa Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi;
  - (c) Ameshindwa kuleta taarifa zozote ambazo zinahitajika kuthibitisha makusanyo yake kwa Halmashauri;
  - (d) Atamshawishi mtu yeyote asilipe au atamzuia mkusanya ushuru yeyote kufanya kazi yake;
  - (e) Atashindwa kuhifadhi kumbukumbu na mahesabu yanayohitajika chini ya sheria ndogo hizi;
  - (f) Atadanganya na kuhusiana na kitendo chake hicho ataikoshesha halmashauri mapato kama ilivyokusudiwa;
  - (g) Atamshawishi mtu yeyote asilipe ushuru au kumzuia mkusakusanya ushuru kufanya kazi yake;
- Atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria ndogo hizi na akithibitika kuwa na hatia ya kosa hilo atawajibika kuilipa Halmashauri faini isiyopungua Laki mbili na ushuru aliotakiwa kuilipa au kifungo cha mwaka mmoja.

Kufutwa kwa  
sheria ndogo

22. Sheria ndogo za ushuru wa soko za Halmashauri ya Wilaya ya Muheza za mwaka 2007 zinafutwa.

---

## JEDWALI LA KWANZA

---

### ADA YA VIZIMBA

---

Na.	Aina ya Kizimba	Kiwango cha ada
1.	Matunda na mboga	300/=
2.	Magunia	300/=
3.	Vizimba vya kuuzia kuku	400/=
4.	Nafaka	300/=
5.	Chai na chakula	300/=
6.	Bucha	400/=
7.	Vizimba vinavyozunguka soko	300/=
8.	Tumbaku na chumvi	300/=
9.	vyoo	Kulingana na mshindi wa zabuni
10.	Maeneo ya wazi sokoni	300/=

11.	Vyumba/stoo ndani ya soko	10,000/= , 20,000/=, 30,000/= 40,000, 50,000 na 60,000 kulingana na ukubwa ulioanishwa na Halmashauri
-----	---------------------------	---

—————  
**JEDWALI LA PILI**  
—————

**ORODHA YA MASOKO ANZISHWA**  
—————

<b>Na.</b>	<b>Mahali soko lilipo</b>
1.	Soko Kuu Muheza Mjini Soko la nafaka, Soko la mbogamboga na matunda
2.	Soko la Samaki
3.	Soko la Mitumba
4.	Soko la Majengo
5.	Soko la Amani
6.	Soko la Michungwani
7.	Soko la Mtindiro
8.	Masoko mengine yakakayoanzishwa na Halmashauri



—————  
**JEDWALI LA TATU**  
—————

**HALMASHAURI YA WILAYA YA M**

—————  
**HATI YA KUKAMATA MALI NA KUIUZA**  
—————

[Limetengenezwa chini ya Sheria Ndogo ya 10]

**JINA LA MALI:** .....

**KWA DALALI WA MAHAKAMA**

.....  
.....  
.....

Hii ni kukuamuru kukamata na kuitunza mali inayoondosheka ya ..... ambayo imeonyeshwa katika Jedwali, mpaka mtajwa hapo juu atakapolipa shilingi..... zikiwa ni deni la kodi analodaiwa pamoja na riba kwa kiwango cha asilimia moja [1%] kwa kila mwezi kuanzia tarehe..... mwezi..... Mwaka. .... Mpaka tarehe.....mwezi..... mwaka..... ikiwa ni pamoja na gharama za kukamata mali hiyo. Na baada ya kutoa taarifa [notice] ya siku kumi na nne ambayo itabandikwa katika jengo la mahakama na baada ya kumalizika kwa notisi hiyo, mauzo ya mali hiyo yataanza kwa mnada ili kupata shilingi.....pamoja na riba na gharama za kukamatia mali hiyo.

**UNAAMRIWA** kurudisha hati hii mnamo au kabla ya tarehe..... mwezi..... mwaka..... Pamoja na maelezo ya namna ulivyotekeleza amri hiyo au sababu kwanini hukutekeleza.

Imetolewa na mimi na kugongwa mhuri wa Mahakama leo tarehe.....  
Mwezi..... Mwaka.....

.....  
**HAKIMU**

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 31 mwezi wa 10 Mwaka 2012 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....  
IBRAHIM M. MATOVU  
MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA  
MUHEZA

.....  
AMIR A. KIROBOTO  
MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA  
MUHEZA

NAKUBALI

.....  
MHE. MIZENGO P. PINDA  
WAZIRI MKUU

DODOMA.  
Tarehe.....